
MEI MMXXIV-TOLEO LA XXXII

# NGURUMO

*ya mwandishi*



## Itambue Furaha

## YALIYOMO

**TAHARIRI**— Itambue Furaha —Uk 02

**MWANDISHI WETU**— ERICK MBISE — Uk 03

**New In Town:** BIMA YA PENZI **—** uk 04

**PITIO LA VITABU**— DIWANI YA KIMBUNGA '4'—Uk 06

**MAKALA**— **SAIKOLOJIA**: Tafuta Upekee Wako —Uk 06 na 07

**MAKALA:** Ziko wapi riwaya za kudumisha historia zetu?**—**uk 08

**MIAMBA WA AFRIKA:** Muammar Gaddafi '07'— Uk 10

**Sako kwa Bako–** Shujaa Maneno: Mvuvi Mvivu**—**Uk 11

**RIWAYA:** — SHAJARA YA MUUAJI '3'—Uk 12 na 13

**RIWAYA—** Cronoc 7 '14'**-** Uk 14 na 15

**YA KALE NI DHAHABU**: — Alibaba na Wezi 40 '11'- Uk 16

**HABARI:** Simulizi Club yamwaga 'maokoto' – Uk 17

**SHUBAKA LA VITABU:** RAFU ya Fadhy Mtanga —Uk 18

**KITABU NILICHOSOMA:** — WHO WILL CRY WHEN I DIE '2'—Uk 19

**MATANGAZO: -** Uk20

**MALENGA WA KILEO —** Uk 21

**HABARI PICHA: -** Uk 22

**KUTOKA MAKTABA:** Maisha ni Mapambano '1'-Uk 23 (Marudio)

**ELIMU JAMII:** — Ukamataji, aupekuzi na Dhamana ya Polisi '3' — Uk 24 na 25

**NGURUMO YA MWANDISHI**

**WASILIANA NASI**
**0766 974 865 AU 0627160016**
**WhatsApp: +255 766974865**

## TAHARIRI:
## Itambue Furaha...

Wasalaam,

Ni mimi mjoli wenu, niko tena hapa mbele yenu, kuwaletea raha yenu ile muisubiriyo kila uanzavyo mwezi.

Naam, hii ndiyo furaha yenu, na najua kuwa mmeitambua ndiyo maana mnaipenda. Na toleo hili la 32 basi "Itambue Furaha". Ndiyo, Ngurumo ya Mwandishi ni furaha yako, umeitambua. Maana ndani yake utapata burudani zote upendazo hasa zile za kifasihi nk. Lakini furaha ni nini? Ngoja nijaribu kukuelewesha maana haya ni mambo ya kisaikolojia wanayajua akina Neema Mgao.

Furaha ni ile hali inayokufanya mtu ujisikie baridi ndani ya moyo, ujione uko mbali na matatizo, ni hali inayotokea baada ya ubongo wako kuona au kusikia kitu ambacho kipo "chanya sana" hahahahaaaaa! Ngumu kweli kueleza. Ukiwa na furaha huwezi kufanya jambo lolote baya katika wakati huo ama juu yako au kwa mwingine. Tambua siku zote ni kitu gani kinakupa furaha, kiishi. Huzuni si mbaya, kwa sababu ili ile hali iwe furaha basi huzuni lazima iwepo.

Mwezi uliopita niliskitika sana kusoma habari ya watu wawili waliojinyonga. Siwalaumu au sijiulizi sana sababu ya kujinyonga kwao ila nilijikuta natafakari kuwa fikra zao, huzuni zao zilikuwa na uzito gani ukipimisha na furaha yao mpaka waone ulimwengu si kitu? Nilijifunza kwamba twapaswa kuwa furaha kwa wengine, kivipi? Tuwafikie wengine, tuingie ndani ya shida zao, tuishi pamoja nao, tugawane maumivu yao. Kama hawa niliosikia habari zao, wangepata watu ambao wangeelewa kile wanachopitia na kuzungumza nao, wasingefikia huko.

Hakuna binadamu aliye kamili, sote tunashambuliwa na shida zilezile, matatizo yaleyale. Lakini Mungu hawezi kuruhusu shida au tatizo lililokuzidi uwezo likupate. Never! Daima Mungu huruhusu tu shida au tatizo ambalo lipo ndani ya uwezo wako kulitatua. Yatupasa kujifunza kubeba na kupambana na malimwengu yanayotuzunguka. Tutajifunza wapi? Yatupasa kusoma sana juu ya saikolojia, yaani vitabu au majarida yanayoeleza mambo anuai juu ya saikolojia ya mtu katika kupambana na matatizo iwe ya kiuchumi, magonjwa, mapenzi, ndoa na familia nk. Kila uga kati hayo una wataalam wake. Kama ni uvivu kusoma basi onana na wataalam washauri wakushauri jinsi ya kupambana na hali hiyo. Usikubali kufa peke yako wakati wapo watu wa kukukwamua ulipo.

Ukiwa na furaha, utaishi miaka mingi sana. Sasa kwanini usiwe na furaha? Nenda kasikilize live band, jichanganye na watu popote walipo, usibaki peke yako. Ukitaka ushauri zaidi wa hayo basi Ngurumo ya Mwandishi tuna Msaikolojia wetu, Neema Mgao atakusaidia.

Karibu!
***Richard Mwambe...***

# MWANDISHI WETU:
# Erick Obedi Mbise



**Toleo hili la 32 katika safu yetu tukufu ya MWANDISHI WETU, tupo na kijana mmoja machachari hivi. Erick Mbise, kama atakavyojieleza mwenyewe. Ni mmoja wa waandishi makini sana katika uga huu wa fasihi. Inaweza kuwa hujamjua, lakini kwa kupitia safu hii utamjua na umsome…**

**Msome sasa umjue, na kisha tafuta kazi zake uhakikishe haya… Karibu**



Naitwa Erick Obedi Mbise, natokea Arusha. Ni mwalimu wa wanafunzi wenye uhitaji maalum katika kitengo cha ulemavu wa akili.

**HISTORIA FUPI KUHUSU SAFARI YANGU YA UANDISHI**

Nikiwa shule ya msingi nilipenda sana kusimulia hadithi kwa wanafunzi wenzangu na niliweza kukusanya wanafunzi wengi muda wa mapunziko kuwasimulia hadithi. Baadae nikawa navutiwa na kusoma vitabu vya hadithi vikiwemo vitabu vya Erick Shigongo. Nakumbuka nilivyoanza kidato cha tano nilianza kuandika stori za kubuni katika karatasi kisha nikawa naziweka sehemu moja.

Baadhi ya wanafunzi wenzangu waliosoma zile stori walivutiwa sana. Wakimaliza kusoma moja wanaomba nyingine. Japokuwa nilikuwa naandika lakini nilikuwa sijawahi kuwaza kuwa mwandishi wa vitabu nilikua tu naandika kujifurahisha na kuwapa wengine wasome. Mwaka 2018 Niliandika kitabu kiitwacho ITAMBUE FURAHA hakikua kitabu cha hadithi ila kilihusu zaidi mambo ya kisaikolojia. Nilianza kuchapa vitabu vitano Sationery iliyokua pembeni ya Chuo.

Ndani ya huo mwaka nikaanza kuandika hadithi katika mtandao wa Whatsapp katika kipengele cha status watu wengi wakavutiwa mwenyewe nikahisi napata furaha zaidi kuandika hadithi za kubuni na hapo ndipo ukawa mwanzo wa kuandika Riwaya. Nitoe shukrani za dhati kwa Hassan Mboneche aliyeniunganisha na wachapaji wa vitabu na kunipa ushauri kila hatua.

**MSUKUMO WA KUWA MWANDISHI.**

Nilipata msukumo wa kuanza kuandika kitabu kulingana na hali niliyopitia binafsi kipindi natafuta Chuo na kuomba mkopo. Nilipitia kipindi cha msongo wa mawazo baada ya kuona kuna mambo hayaendi kama nilivyotarajia. Nilianza kujifunza juu ya kuwa na furaha na nikapitia majarida na vitabu namna ya kupata furaha. Baadae hali ilirudi kuwa sawa ila nikapata msukumo wa kuandika kwaajili ya wengine waliokua wanapitia hali ya kukosa furaha kutokana na hali mbalimbali. Chuoni nilikua nasoma masomo ya saikolojia pia, hivyo nikawa napata mawazo ya kitaalamu zaidi. Baadae niliendelea na uandishi wa hadithi na niligundua watu wengi wanapenda hadithi kuliko vitabu vya mafundisho.

**UJUMBE KWA WAANDISHI WENZANGU NA WASOMAJI.**

Tusikate tamaa kazi za uandishi zina changamoto nyingi hususani kwa waandishi wachanga. Pili tuwe na mawazo ya kuona mbali na kuifikia Dunia, binafsi nimefanikiwa kuuza nakala nyingi Marekani, Ujerumani na Australia lengo ni kuuza kitabu kila bara. Hili linawezekana kwa kuandaa kazi kwa Lugha zaidi ya moja mfano ukitoa nakala kwa lugha ya kiswahili unatoa pia kwa lugha ya kiingereza. Wasomaji ni nguzo muhimu kwetu kuendelea kuandika bila msomaji mwandishi atakata tamaa.

Vitabu vya ERICK MBISE

**RIWAYA**

1. SITAKUACHA OBADIA
2. NITAKUONA TENA,
3. SANDUKU JEUSI
4. CHOZI LA MWISHO with English Version THE LAST TEAR.

Kitabu cha mafundisho kimoja
ITAMBUE FURAHA.

**Vitabu vinapatikana Arusha nje ya Jengo la kimahama bookshop kwa wakala Ally Said au kwangu kupitia mawasiliano ya 0764016589, 0673016589.**

## NEW IN TOWN :
## BIMA YA PENZI (RIWAYA NA PIA BIMA HALISI)

**USULI.**
Mapenzi kwa lugha nyingine mahusiano, ni sehemu muhimu sana ya maisha ya mwanadamu kote ulimwenguni. Umuhimu wake unakuja kutokana na ule ukweli kwamba kila mmoja aliyekaa juu ya uso wa dunia, mwenye hisia na mahaba basi atayakuta na atayapitia, ataishi nayo iwe kwa heri au kwa shari.

Watu wengi wamepita katika mapenzi na kuathiriwa vibaya, wakajikuta katika wimbi la usaliti, ulaghai, uongo na mengine ambayo yamepelekea athari mbalimbali kama vile vifo, maradhi ya sukari, moyo, msongo, sonona na afya ya akili.

Kwa mujibu wa taarifa ya vyombo vya Habari kama vile mtandao wa wa BBC https://www.bbc.com/swahili/61655800. Ulikuja na Habari zilizoonesha athari za mapenzi katika jamii za kitanzania. (Rejea Yusuph Mazimu BBC Swahili 1 Juni 2022 aliyeandika "Mauaji ya wivu wa kimapenzi Tanzania, yalianza kama kipele sasa ni jipu la kutumbuliwa"
Taarifa ilieleza pia ya kuwa katika mwezi sepetember tu mwaka 2022 matukio 14 ya vifo vinavyotokana na wivu wa mapenzi vilitokea. Kwa mwaka huohuo 2022 wastani wa vifo 20 kwa mwezi viliripotiwa. Hii karibu vifo 240 kwa mwaka.

Huku Mwananchi Mtandaoni kupitia mwandishi wake George Helahela The Citizen Data Reporter Mwananchi Communication Limited liliripoti ya kuwa "Wivu wa mapenzi mzimu mpya wa vifo vya mauaji Afrika Mashariki"
Jumanne, Novemba 01,2022 https://www.mwananchi.co.tz/mw/habari/kitaifa/wivu-wa-mapenzi-mzimu-mpya-wa-vifo-vya-mauaji-afrika-mashariki-4004422


Bado vyombo vya Habari viliendelea kuripoti juu ya madhara ya mapenzi na wivu ambapo mwanachi iliripoti juu ya "Wivu wa mapenzi kupitiliza, tatizo la afya ya akili" hii ilikuwa Jumatatu, Oktoba 18, 2021

**TAFAKURI YA KINA JUU YA UMUHIMU WA BIMA YA PENZI AMA BIMA YA MAHUSIANO**

Kama binadamu tunaofikiri sawa sawa, Mara kadhaa tumejiuliza kwa nini hakuna bima ya penzi ambayo itasaidia kupunguza na pengine kuondoa kabisa hizi changamoto na athari ambazo zimeendelea kutuachia makovu kila uchao.
Pamoja na sababu lukuki zinazoweza kuwekwa mbele, sisi kama Taifa ni muhimu kuwaza tena haswa katika maeneo ambayo yatakwenda kupunguza majanga ya mahusiano kila leo katika jamii zetu.

Baadhi ya sababu muhimu za kuanzisha bima hii muhimu ni pamoja na kujipatia unafuu wa kupata matibabu kwa mujibu wa mahitaji ya mkata bima.
Kupata mapumziko/ahueni katika kipindi za mpito ikiwa mmoja ataamua kuyapisha mahusiano mpaka kipindi ambacho akili yake itakuwa imetulia ili kuupisha ubungo kufanya jambo jingine.

Msaada wa huduma za kisheria haswa dhidi ya wale ambao wanafikia katika hatua ya kuachana bila kuelewana na hivyo kupelekea Kwenda kwenye vyombo vya haki.
Ziara za mapumziko ili kupisha upepo mbaya kipindi cha kuachana.
N.k
Sisi tunaamini bima ya penzi/mahusiano ni tiba mujarabu kwa jamii zetu kwa kuwa hakuna njia ya kuepuka mahusiano bali kuyakabili.





- Mwandishi anaitwa Mwamwingila Goima (Mwamwingila G.P) ni Mtanzania, mwalimu na Gwiji wa fasihi ya Afrika.

- Ni mwanachama wa UMOJA WA WAANDISHI WA VITABU TANZANIA (UWAVITA) na ndiye aliyekuwa mwenyekiti wa kamati maalumu iliyofufua umoja wa waandishi wa vitabu Tanzania.

**NB: Tembelea www.getvalue.com upate nakala yako**

# KITABU: KIMBUNGA (DIWANI) - 4

**PITIO LA VITABU**




***Inatoka toleo lililopita...***

Ukoloni mamboleo unawaathiri watu wa tabaka la chini wasio na chochote na kuwanufaisha matajiri au tabaka la juu. Katika ubeti wa 6 mwandishi anasema:-

"*Ambao ni matajiri, kwao anapowafikiya,*

*Huweza kujisitiri, salama kujipatiya,*

*Walokuwa mafakiri, huzidi kuwaoneya*

*Huyu ndiye Chuwi gani?*

Mwandishi ameeleza kuwa ukoloni mamboleo huingia kwa njia mbali mbali katika nchi zinazoendelea. Hivyo mwandishi anatahadharisha kuwa tuepukane na mbinu (njia) hizo na tuupinge ukoloni mambo leo kwa nguvu zote ndipo tutaweza kujenga jamii mpya.

**5. Umuhimu wa kujitawala**

Ili tuweze kujenga jamii mpya ni lazima tujitawale katika nyanja zote za kifikra, kisiasa, kiutamaduni pamoja na kiuchumi. Katika shairi la "Afrika "Mwandishi anaeleza kuwa ili tuweze kujitawala ni lazima tuepukane na unafiki, vibaraka (wasaliti), tusikate tamaa na tudumishe amani. Katika ubeti wa 3 msanii ansema:-

*"Wasaliti wazikishe, wasiwe wenye kuzuzuka,*

*Tamaa uwakatishe, yasiwe wanayotaka,*

*Katu wasiwawezeshe, wabakiye kuzuzuka,*

*Washindike mahusuda, wasopenda bara letu."*

Katika shairi la "Kujitawala" Mwandishi anaeleza umuhimu wa kujitawala kwa jamii yoyote ile. Mwandishi anaonesha kuwa, kujitawala ni pale umma unapokuwa na mamlaka ya kuamua mambo yao wenyewe bila kuingiliwa au kuwekewa vikwazo vyovyote. Katika Ubeti wa 1 Msanii anasema:-

*"Kujitawala si kwema, kuliko kutawaliwa,*

*Kujitawala ni umma, kila yao kuamua,*

*Kujitawala si kama, ulanguzi na rushwa*

Katika shairi hili la 'kujitawala' mwandishi anaonesha faida mbalimbali za kujitawala kama vile kuwepo kwa demokrasia, kuwepo umoja na ushirikiano, kuwepo haki na usawa, amani hudumishwa, vile vile mila na desturi za nchi zinadumishwa. Hivyo mwandishi anatuasa kuwa ili tujenge jamii mpya ni lazima tujitawale kisiasa, kiuchumi, kiutamaduni na kifikra.

**6. Umuhimu wa kazi na kuwajibika**

Kazi ni nguzo muhimu sana ya ujenzi wa jamii mpya. Mwandishi amesisitiza umuhimu wa kazi na kuwajibika katika shairi la "Kazi" Mwandishi anatuonesha kuwa kazi ndio msingi wa maendeleo. Anasisitiza umuhimu wa kufanya kazi kwa bidii na tuepukane na njaa. Ubeti wa 1,mwandishi anasema;-

*"Pesa huletwa na kazi, ni njia zipitiayo,*

*Hutopata matumizi, iwapo kazi hunayo,*

*Hata njaa hukuhizi, uvivu na angamiyo"*

Katika shairi la "Uokolewe",mwandishi anasisitiza umuhimu wa kudumisha umoja na mshikamano ili kuinua uchumi wetu. Anasisitiza umuhimu wa kufanya kazi kwa bidii na kutumia vyema rasilimali zetu ili kuinua uchumi wetu.

Katika shairi la "Dumizi" mwandishi anakemea tabia ya baadhi ya watu kukaa bila kazi (uvivu) na kuanza maisha ya kunyonya. Hivyo mwandishi anapiga vita unyonyaji unaofanywa na baadhi ya watu.

Hivyo msanii aniasa jamii kujihusisha na ukulima, uvuvi, utalii na viwanda ili kujenga jamii kwa upya.

**7. Mapenzi na ndoa**

Katika diwani hii, mwandishi ameonesha kuwa mapenzi yamegawanyika katika pande kuu mbili ambazo ni; Kuna mapenzi ya kweli na mapenzi ya udanganyifu.

Katika shairi la "Usimpige Mkeo " mwandishi anasema kuwa haifai mwanaume kumpiga mke wake na vile vile mwanaume hatakiwi kumwekea mkewe masharti magumu.

***Itaendelea toleo lijalo...***

# -SAIKOLOJIA-

## TAFUTA UPEKEE WAKO, RINGIA NA UUTUNZE HUO

**Neema Mbilinyi Mgao**

**0763013206.**
**Karibu.**

**The magic author.**



U hali gani mpenzi msomaji wa jarida la NGURUMO YA MWANDISHI, hasa makala hii ya Saikolojia?

Mwezi huu katika makala hii tunaangazia upekee wako wewe, Ama waweza sema utofauti wako wewe na wengine.

**Nini maana ya upekee?**
Upekee ni zile tabia zako binafsi au ule u-wewe wako binafsi. Au waweza tafsiri kama ni zile taratibu ulizonazo wewe katika kuendesha mambo yako binafsi ambazo huwa tofauti na mwingine.

**Utaujuaje utofauti wako?**
Utofauti au upekee wako kama nilivyosema pale mwanzo kuwa ni ile hali ya namna yako katika kutatua mambo yako, Sasa utaujuaje upekee wako, ni rahisi sana, kwanza vumbua ugunduzi wa tabia zako ambazo mnatofautiana na mwingine, yaani unaweza kukuta furaha yako wewe baba sio kuwa ndiyo hiyo furaha ya mtoto uliemzaa. Kwamba furaha yako wewe mke sio sawa na furaha ya mumeo. Kwamba hata ile hasira yako sio sawa na ilivyo hasira ya mtu mwingine.Ule uwezo wa kuchanganua mambo sio sawa na uwezo wa mtu mwingine.

**Upekee hupatikanaje?**
Upekee hupatikana kutokana na mambo haya yafuatayo.

**1.Karama kutoka kwa Mungu.**
Mungu anapomuumba mwanadamu humpa na karama zake binafsi, ikijumuishwa na tabia binafsi. Hivyo chanzo kikuu cha upekee hutoka kwa Mungu. Mungu alimuumba kila mmoja kwa upekee wake na tabia zake.

**2. Malezi utakayolelewa.**
Chanzo kingine cha upekee ni vile mtu anavyolelewa. Mzazi au mlezi, anayo nafasi ya kumtengenezea yule anaemlea tabia zake binafsi, au upekee wake. Mzazi au mlezi anayo maamuzi ya kuamua mtoto aweje, yanayowezekana kwa kudra za Mungu yanabakia kwa Mungu lakini yanayoweza kutengenezwa na mzazi au mlezi basi yatengenezwe.

**3.Kuelimishwa.**
Hii hupatikana zaidi mashuleni, lipo kundi ambalo ni la muhimu sana katika kutengeneza upekee, nalo ni kundi la waalimu.Waalimu wanayo nafasi kubwa katika kuitengeneza tabia binafsi ya mtu. Waalimu wanayo nafasi kubwa kumtengenezea upekee mtoto katika ukuaji wake.

**4. Kujitengenezea.**
Hapa ndipo kwenye kiini cha mada yetu siku ya leo. Kujitengenezea upekee, hatua hii ndio ya muhimu sana, inakusanya vile vyanzo vitatu vya upekee kule juu na kuvileta hapa. Mtu huweza kujitengenezea upekee kwa kukusanya matukio yote aliyopitia na kuamua kujiumbia hatua au tabia mpya au upekee wake. Hatua hii ndio tunampata mtu kamili sasa kwani atakua amebarikiwa na karama ya tabia alizopewa na Mungu, akapewa na zile alizolelewa, na akapewa na zile alizofunzwa shuleni. Na kadri mtu huyu anavyokua na kupangua yale anayokutana nayo basi anajitengenezea na upekee wake.

Upekee wa mtu katika mambo mengi yanayomzunguka hutokana na mambo hayo manne, lakini kubwa ni kuwa upekee unapokua mtu mzima unautengeneza na kuulinda wewe mwenyewe bila kuruhusu mtu au watu wauondoe. Zilinde sana tabia zako, ulinde sana upekee wako. Kwa kuruhusu tabia za mtu mwingine zikubadilishe ni wazi kuwa utaishi katika nafsi ya mtu mwingine ikiwa ndani yako, kwani utaishi atakavyo mwingine, na sio upendavyo wewe. Maana uwewe wako umeuacha, unaishi kwenye matakwa ya mwingine.

**UTAUGUNDUAJE UPEKEE WAKO?**
Ugunduzi wa upekee wako ni pale unavyofanya mambo tofauti na wengine, hasa katika haya yafuatayo.

# -SAIKOLOJIA-
# TAFUTA UPEKEE WAKO, RINGIA NA UUTUNZE HUO

**A. Hasira.**
Upekee wako tutauona pia pindi ukikasirika. Kuna mtu akikasirika anatetemeka sana kiungo fulani cha mwili, mfano: mtu mmoja alikuwa akitetemeka mikono pindi anapoudhiwa. Yaani akikasirika basi utakuta atapiga mtu mpaka aone damu ndio atulie. Utakuta mwingine akikasirika yeye anashikwa na usingizi anaenda kulala. Huo ni upekee wa watu wawili tofauti.

**B. Furaha.**
Kuna mwingine akifurahi hadi analia. Mwingine akifurahi anacheza sana muziki, sasa ukute mtu huyo akifurahi furaha yake ichagizwe na kitu kingine kama kileo n.k. Mwingine akifurahi anapiga kelele sana, basi mtu atafurahi kwa kipimo chake.

**C. Utatuaji wa matatizo.**
Mahali pengine pa kuutambua upekee ni katika utatuaji wa matatizo, mwingine akikumbwa na tatizo anakurupukia maamuzi na kulipuka, lakini mwingine akikumbwa na matatizo anatulia kabla ya kufanya maamuzi.

**UTAUTUNZAJE UPEKEE WAKO?**
Kwanza kabisa tambua kuwa upekee ni lazima uutunze na uulinde. Hizo tabia zako binafsi, zinazokutofautisha na wengine ni lazima uzilinde, usiishi kiunafiki kwamba ukiwa na rafiki mwenye tabia hizi unabadilika, ukiwa tena na rafiki mwenye tabia zile tena unabadilika.

Sasa utabadilika mara ngapi? Maana kila iitwapo leo tunabadilisha marafiki kulingana na sababu moja au nyingine. Inawezekana ukawa na rafiki mlevi leo, basi na wewe ukaanza ulevi, kesho ukampata rafiki mlokole  na wewe ukaokoka, keshokutwa ukapata rafiki yeye ni bingwa wa kukopa, na wewe ukaanza kuwa mtu wa mikopo. Jamani, jamani, si utaiyumbisha Saikolojia yako.

Usiishi kwa mkumbo. Jambo jingine, usifate vile wanavyoishi wengine, ishi ukiulinda upekee wako, ishi ukisimamia misingi uliyojiwekea, misingi uliyowekewa. Na misingi uliyojiwekea ndiyo hukutambulisha wewe katika utofauti wako na mimi.
Linda saana upekee wako, usikubali ukayumbishwa aidha na mazingira au na jambo lolote.

**UFANYE NINI IKIWA UPEKEE WAKO UMEUTETERESHA.**
Upekee wako hutatereshwa na wewe mwenyewe. Ikiwa utapata nafasi ya kugundua kuwa upekee wako umeuteteresha basi shukuru Mungu kuwa umepata neema ya kutambua uteremshwaji wa upekee wako. Wapo watu wametetereka na bado hawajagundua kama wametetereka. Hivyo ikiwa utagundua kama umepoteza upekee wako basi cha msingi rudisha kumbukumbu nyuma na ukagundue pale ulipouacha upekee wako. Ukishaukumbuka basi uchukue endelea kwenda nao, hiyo ndio tofauti yako na wengine itunze.

Jambo jingine la umuhimu ni kumuomba Mungu kwa imani yako. Mwombe Mungu akulinde ili uweze kuutunza huo upekee wako. Kuna wakati upekee wako utakutenga na watu wako wa karibu, watakuona kama una msimamo sana, kama una itikadi sana, lakini pengine huo msimamo wako utakusaidia wewe kuwa na maisha mazuri. Chukulia mfano upekee wako wa kujiepusha magomvi, ule una hasara?.
Mwombe Mungu, yeye akulindie upekee.

Asante saana, karibu saana kwa mazungumzo  ya binafsi. Kuliko ukumbwe na matatizo hata ujiue, kuliko ukumbwe na wivu wa mapenzi hadi uue, basi karibu tuzungumze.

Nipigie kupitia +255763013206. Shukrani.

**Madame Neema Mbilinyi Mgao.**

**Dodoma.**
**Tanzania.**

# MAKALA: Ziko wapi riwaya za kudumisha historia zetu?

Na Markus Mpangala

Baruapepe; mawazoni15@gmail.com/ WhatsApp; 0719 226293.

MWEZI Aprili mwaka huu nilikuwa natazama filamu moja ya kusisimua. Nakiri sijawahi kuona filamu ya aina yake inayotukuza mila,desturi, utamaduni za jadi za Afrika na zaidi kutunza historia ya jamii hapa duniani, tena ikitoka katika Taifa kubwa lenye nguvu kijeshi,kiuchumi na maendeleo, Marekani.
Katika filamu hiyo kuna simulizi za Ufalme wa Songhai na Mali (ambazo wanafunzi wengi wa Tanzania wamesoma katika shule za sekondari. Simulizi zinaonesha juu ya utawala wa Malkia mmojawapo aliyesababisha Dola yake kuangushwa kutokana na kuingia vitani.

Ndani ya filamu hiyo, Malkia huyo anaonesha jinsi alivyoingia vitani na kuupiganisha umalkia wake na utawala wa majirani. Katika vita vile utawala wa Malkia huyo ulipigwa vibaya sana na kuangushwa kisha kuichupua uongozi mwingine. Katika filamu hiyo ambayo inamilikiwa na kampuni ya Marekani imeonesha namna simulizi za jadi zinavyoweza kutumika katika fasihi pamoja na kulinda historia ya jamii na nchi.

Aidha, ujumbe mwingine tunaopata ni matumizi ya teknolojia ya kisasa kulinda utamaduni,mila,desturi na historia ya jamii kwa ujumla wake. Katika fasihi andishi na simulizi zote zina dhima moja ya kuhakikisha historia ya mahali,jamii na mengine zinalindwa. Filamu humika kufikisha ujumbe haraka na kuhifadhi kumbukumbu. Hali  kadhalika fasihi andishi hutumika kufikisha ujumbe huo na kuelezea mazuri ya kihistoria ndani ya Mataifa yetu.
Hapa nchini Tanzania, waandishi wa kazi Bunifu wamefanya vizuri katika kuenzi fasihi, kuleta ladha ya kisasa pamoja na wengine kukumbusha ya zamani. Mathalani katika ladha za riwaya za E.A Musiba nyingi zinaonesha juu ya siasa za ukombozi,uhuru wa mataifa ya Afrika,ujasusi,diplomsia pamoja na umuhimu wa mshikamano. Katika eneo hili ndipo riwaya ya "Mpatanishi" iliyoandikwa na mwandishi bunifu Richard Mwambe ama maarufu kama Kamanda Amata. Huyu amepita njia ya uandishi wa E.A Musiba na Ben Mtobwa. Mpatanishi ni miongoni mwa riwaya zinazohamasisha uzalendo kwa nchi.

Aidha, riwaya za Ben Mtobwa zilikuwa zimejikita kwenye maudhui ya hujuma. uhalifu, ukosefu wa uzalendo,siasa chafu,ufisadi na kuporomoka kwa maadili. Hata hivyo licha ya waandishi hao wawili kuwa dira, lakini waandishi wa kizazi chetu wameshindwa kugundua udhaifu wa wazee wetu. Ukiondoa Fadhy Mtanga, mwandishi bunifu ambaye husifika kwa kuelezea mitaa na miji ya wahusika wake kwa ustadi wa hali ya juu bado ipo changamoto kwa wengine kutunza historia zetu.

Kwenye riwaya za waandishi bunifu wa kizazi hiki kumekuwa na upungufu wa simulizi za kihistoria. Mfano mwandishi katika masuala la burudani anaweza kuzungumzia kumbi za starehe za muziki (udhaifu ambao umo katika kazi za wazee wetu waliotajwa hapo juu), lakini hakuna anayejaribu kuelezea taswira ya kumbi za ndondi za akina Rashid Matumla, Michael Yombayomba na wengineo kwa nia ya kuenzi historia za michezo.

Vilevile simulizi za riwaya za kizazi cha kisasa zinawapunja wasomaji wa nyakati hizi kupata uhondo wa mila na desturi mfano za lugha za makabila,ngoma na tamaduni nyinginezo nzuri ili kuzilinda na kuenzi maisha yao. Waandidhi wetu wanapaswa kuwalisha wasomaji juu ya kumbukumbu za historia, iwe mbuga, uongozi,siasa,michezo na burudani ama mengine kama simulizi za wazee wetu zenye tija na muhimu kulindwa.

Ni muhimu kutambua kuwa kizazi chetu kinaishi katika nyakati za teknolojia ambapo masimulizi mengi yamejikita katika vifaa vya mawasiliano na uvumbuzi wa nchi za magharibi. Wakati kampuni kubwa za filamu na fasihi zikihangaika kutumia teknolojia hiyo kulinda na kuenzi historia, mila na desturi za Kiafrika na kuziuza machoni pa wanajamii wao na kwetu, lakini hapa kwetu tumetelekeza historia hizo wala hatujigusi hata kwa kuzungumza na wazee juu ya mazuri ya kimila, desturi na historia za mahali. Napenda kutoa changamoto kwa watunzi kote nchini.

**Mzee wa Lundu**


The Grand Kagera-Tour
THE GRAND
KAGERA MARATHON
Kutakuwa na Mashindano ya Mbio tarehe 06/07/2024 katika Wilaya ya Karagwe, kutakuwa na Mbio za Km 21, Km 10, Km 5. Kwa Kiingilio Cha 15,000/=, na VVIP 40,000/= Kwa Km 2, Mbio hizi zitashirikisha wasanii maarufu kutoka Dar es Salaam.
JUMAMOSI
06 JULY, 2024
MBIO ZITAANZA
07:00 ASUBUHI - 06.00 MCHANA
KAGERA
KARAGWE
JISAJILI SASA
Pesa zitakazopatikana tunachangia vifaa vya kujifungua Kwa wanawake walioko magereza ,na kujenga makumbusho kagera
Lipa namba M-PESA 54279896
SEPENGA ENTERTAINMENT LIMITED
Kwa mawasiliano
0696 972 772


JAMVI LA SIMULIZI
MOBILE BOOKSHOP
VUKA UJANA
SALAMA Inawezekana
FURAHA A KABAGE
VUKA UJANA
SALAMA
inawezekana
Tupigie/WhatsApp
0766974865
MPESA LIPA NAMBA
5559006
JAMVI LA SIMULIZI
Tsh
10,000
•Tunapatikana Gangilonga, Allamano Centre pembeni mwa Chuo Kikuu Huria - IRINGA


SEPENGA ENTERTAINMENTS
The Grand Kagera-Tour
2, 5, 10, 21 KILOMETERS
MARATHON
EVENT
Kutakuwa na Mashindano ya Mbio tarehe 06/07/2024
katika Wilaya ya Karagwe, kutakuwa na Mbio za Km 21, Km 10, Km 5. Kwa Kiingilio Cha 15,000/=, na VVIP 40,000/= Kwa Km 2, Mbio hizi zitashirikisha wasanii maarufu kutoka Dar es Salaam.
06 JULY
7 AM
KUSHIRIKI MBIO HIZI
Lipa namba M-PESA 54279896
SEPENGA ENTERTAINMENT LIMITED
Pesa zitakazopatikana tunachangia vifaa vya kujifungua Kwa wanawake walioko magereza ,na kujenga makumbusho kagera
Kwa mawasiliano
0696 972 772
KAGERA - KARAGWE


IGP 'Kamari Ya Roho'
Tsh 4000 UPDF
lipa kwa
Mpesa Lipa Namba
5559006
JAMVI LA SIMULIZI
WhatsApp +255 766 974865
Kamanda Amata
IGP



Muamar Muhammad Abu Minyar Al - Gadafi

Inaendelea...

Mnamo Mei 1970, Semina ya Wasomi wa Mapinduzi ilifanyika ili kupata wasomi kuendana na mapinduzi, wakati Mapitio ya Sheria na Marekebisho ya mwaka huo yaliunganisha kanuni za sheria za kilimwengu na za kidini, kutambulisha sharia katika mfumo wa sheria. Ikitawala kwa amri, RCC ilidumisha marufuku ya kifalme kwa vyama vya kisiasa, mnamo Mei 1970 ilipiga marufuku vyama vya wafanyikazi, na mnamo 1972 iliharamisha migomo ya wafanyakazi na kusimamisha magazeti.

Mnamo Septemba 1971, Gaddafi alijiuzulu, akidai kutoridhishwa na kasi ya mageuzi, lakini alirudi katika nafasi yake ndani ya mwezi mmoja. Mnamo Julai 1972, huku kukiwa na uvumi ulioenea kwamba Gaddafi alifukuzwa au kufungwa jela na wapinzani wake wa kisiasa, baraza jipya la mawaziri la watu 18 liliundwa na wawili tu kati yao, Jalloud na Abdel Moneim al-Houni, wakiwa wanajeshi; wengine walikuwa wanateknolojia wa kiraia kulingana na msisitizo wa Gaddafi. Mnamo Februari 1973, Gaddafi alijiuzulu tena, akarudi tena mwezi uliofuata.

**Mapinduzi Maarufu: 1973-1977**

Tarehe 16 Aprili 1973, katika hotuba yake huko Zuwarah, Gaddafi alitangaza kuanza kwa "Mapinduzi Maarufu". Alianzisha hili kwa mpango wa hoja tano; ya kwanza ambayo ilivunja sheria zote zilizopo, na nafasi yake kuchukuliwa na sheria za mapinduzi. Hoja ya pili ilitangaza kwamba wapinzani wote wa mapinduzi walipaswa kuondolewa, wakati ya tatu ilianzisha mapinduzi ya utawala ambayo Gaddafi alitangaza yataondoa athari zote za urasimu na ubepari. Hoja ya nne ilitangaza kwamba idadi ya watu lazima iunde Kamati za Watu na wawe na silaha ili kuyalinda mapinduzi, huku ya tano ilitangaza mwanzo wa Mapinduzi ya Kiutamaduni nchini Libya, ili kufutilia mbali nchi hiyo kutokana na ushawishi "sumu" wa kigeni.

Alianza kutoa mhadhara juu ya awamu hii mpya ya mapinduzi nchini Libya, Misri na Ufaransa. Kama mchakato, ulikuwa na mambo mengi yanayofanana na Mapinduzi ya Kitamaduni yaliyotekelezwa nchini Uchina.

Kama sehemu ya Mapinduzi haya maarufu, Gaddafi aliwaalika watu wa Libya kuunda Kamati Kuu za Watu kama njia za kuongeza ufahamu wa kisiasa. Ingawa anatoa mwongozo mdogo wa jinsi ya kuanzisha mabaraza haya, Gaddafi alidai kuwa watatoa aina ya ushiriki wa moja kwa moja wa kisiasa ambao ulikuwa wa kidemokrasia zaidi kuliko mfumo wa uwakilishi wa jadi wa chama.

***Itaendelea...***

**Gaddafi akiwa na Rais wa Romania Nicolae Ceaușescu huko Bucharest, 1974**



# SAKO KWA BAKO:

## SHUJAA MANENO: Mvuvi mvivu, mshairi chipukizi na rafiki wa vitabu

SHUJAA MANENO ni jina langu mimi nililopewa na wazazi wangu. Baba yangu ni mzee Maneno Abdalah mkazi wa Utete Rufiji. Nimezaliwa huko miaka 34 iliyopita.

**Kwanini unajiita Mvuvi mvivu?**

(Anacheka) Nimezaliwa kwenye familia ambayo maisha yake yanendeshwa kwa uvuvi, baba yangu ni mvuvi na kaka yangu mmoja pia. Ijapokuwa nilifundishwa sana kuwa mvuvi lakini kila baba aliponikosa mtoni alijuwa wazi ni wapi nipo.

Nilikuwa napenda sana kusoma vitabu na kusikiliza kipindi cha Malenga wetu RTD wakati ule. Kiukweli sikupenda kuwa mvuvi, sasa mama yangu bibi yangu mzaa baba ndiye alipenda sana kuniita Mvuvi mvivu.

**Baada ya kutopenda uvuvi, ukafanya nini?**

Nilisoma kwa bidii sana ili niondokane na ile hali ya maisha ya uvuvi. Nilifanikiwa kwani nilipomaliza std 7 nikapata shule ya sekondari mpaka form 4 na hapo nikaenda kusomea ualimu.

Mimi ni mwalimu wa somo la Kiswahili, nafundisha shule fulani huku Bagamoyo na makazi yangu ni hukuhuku kijiji cha Ukuni barabarani kabisa.

**Umeoa?**
Hapana, sijaoa, na huu ndiyo ugonvi mkubwa sana na bi mkubwa nyumbani.

**Una mchumba?**
Hapana sina, wala mpenzi sina mi nina aina yangu ya maisha ambayo kwayo napenda kuishi ila nina watoto wawili, Abubakar Shujaa na Fatma Shujaa, wote wanaishi na mama zao, mimi ninatoa malezi na kila kitu. Kwa hiyo najiona tayari nina kila kitu.

**Tuelekee upande wa fasihi na upenzi wa vitabu… tuambie hapo!**

Mimi ni mpenzi sana wa vitabu tangu utoto wangu. Nilipokuwa shule ya msingi darasa la nne na kuja juu, somo la Kiswahili, mimi ndiye nilikuwa kinara wa kusoma zile hadithi mbele ya darasa. Halafu mashairi yale 'Karudi baba mmoja' na 'sizitaki mbichi hizi' nilikuwa napenda kughani kama wafanyavyo redioni wakati ule. Nilikuwa napenda sana, mpaka sasa.

**Kwanini unajiita Mshairi Chipukizi?**
Ninaandika mashairi lakini bado nakwama maeneo mengi sana, maana ushairi unahitaji ulumbi mpana sana wa lugha, ujue kuchezea na kuikunjakunja lugha ili mizani ipimike na vina vitulie.

Upande wa uandishi wa riwaya, sijawahi kuchapa kitabu. Ila nimeandika andika na moja ya kitabu changu kinaitwa MVUVI MVIVU…

Navutiwa sana na uandishi wa Maundu Mwingizi, Fadhi Mtanga na siku hizi huyu nani Dotto Rangimoto.

Mimi si mpenzi wa riwaya za kijasusi kwa sababu sipendi uchokozi. Lakini hapa ninavyo vya Nyong'oro Japheti, kuna kaladha fulani katika kalamu yake huwa nakapenda sana kukasoma.

Umeona tofauti yoyote kati ya waandishi wa zama zile na sasa?
Aaaaa braza! Tofauti ni kubwa mno kubwa kwa sababu wale wa zama zile waliandika sana na walikuwa watafiti hasa, hivyo wale ni bora kuliko wa sasa. Na hawa wasasa wamebweteka kwenye google sana, hivyo utafiti wao wa mambo ni kigugogugo, lakini wana ladha yao ambayo wale wa zama zile hawakuwa nayo, hivyo hawa wa sasa ni bora kuliko wale wa zama zile.

**Shujaa Maneno, tukushukuru kwa yote, nafikiri hiyo riwaya yako ya Mvuvi Mvivu tutapenda isomwe humu…**

Shukrani sana, haina shida. Nami nawapongeza Ngurumo ya Mwandishi mnatuweka karibu sana na waandishi wetu na fasihi kwa ujumla.

RM.

# SHAJARA YA MUUAJI—3

Na. Richard Mwambe



***Ilipoishia...***

***Sajini Steven alifika msibani akiwa na kanzu safi ya Kiislam. Akajichanganya huku na huko ilimradi asikie chochote kinachonenwa na waja. Kila alikokaa alisikia sifa nzuri tu za Sume.***

***Endelea...***

Moyoni mwake akaona kuwa marehemu kwa namna moja au nyingine hakuwa na rafiki wa karibu katika maisha yake. Maana Steven aliamini katika falsafa ya mwanamuziki Bob Marley kuwa ni 'rafiki yako tu atakayejua siri zako, na ni yeye anayeweza kuzianika'. Haikuwa rahisi, aliendelea kuhamahama hapa na pale, haja yake tu asikie nini kinaweza kuwa chanzo cha kifo hicho.

Alipokuwa akienda kujisaidia akakuta kundi la akinamama likimpepea mwenzao aliyelala mchangani. "Yàani huyu dada hii sijui mara ya sita anazimia... Mwisho atatufia hapa!" Kuzimia ni kawaida kwa wanawake misibani hasa kama marehemu alikuwa na ukaribu na mtu huyo. Matatu; ama ndugu wa karibu, au rafiki wa karibu au kimada wake. Ndivyo inavyokuwa. Steven akapita na kwenda kumaliza shida zake, kishapo akarudi kwa kupita palepale.

"Mpeni hewa sasa, msimzunguke!" Akawaambia wale akinamama nao wakatii. "Huyu ni mke wa marehemu?" Akauliza.
"Hapana! Ni mwombolezaji tu..."
"Na mnajua anapoishi?" Akahoji. Kati ya wale wanawake wote hakuna aliyejua mwanamke huyo ni wa wapi. Hakujali, akilini mwake akajenga wazo la kumfuatilia ili tu ajue ni wapi aishipo. Aliona wazi kuwa kupitia mwanamke huyo anaweza kupata A,B na C za marehemu. Msiba ulimalizika na kila mmoja alirejea kunako makazi yake.

❦ ❦ ❦

Siku nne baadae, Amina Kalolo alipokea ugeni nyumbani kwake Ukonga Mombasa. Alikuwa ndani, kimya, hakuwa hata na mpango wa kutoka. Bado moyo wake ulijawa huzuni. Mbisho wa hodi ndiyo uliyomwinua kitandani alipojilaza. "Nani?" Akauliza kwa sauti yake nyororo pindi alipoufikia mlango. Tangu ajifungie humo ndani, hiyo ndiyo ilikuwa hodi ya kwanza. Akafungua mlango kidogo ili kuweza kuona nje. Mbele ya mlango huo alisimama kijana mtanashati. Aliyevalia fulana ya gharama na suruali aina ya kadeti. Vyote vilimkaa vyema na kuudhirisha ushababi wake. Mkato wa nywele zake ndiyo haswa uliomfanya mwanamke huyo kugundua kuwa mgeni wake ni mtu anayejipenda. Ingawa hakujibiwa swali lake la *'nani'* alilouliza kabla hajaufikia mlango, Amina alijikuta akifungua mlango kumkaribisha huyo mgeni. Mwonekano ulimshawishi.

"Karibu ndani!" Alimkaribisha huku akimpisha apite. Mgeni yule akaingia na kujitupa kochini wakati Amina akielekea chumbani kujiweka sawa maana alitoka na shuka tu alilojiviriga mwilini na kulikamatia juu ya kifua chake. Loh! Mitikisiko ya maeneo yake ya nyuma, chini ya mgongo ilimfanya mgeni yule kusisimka mwili. Amina akapotelea chumbani na alipotoka alikuwa ndani ya gauni refu la kitenge lililomwagika mpaka chini, wenyewe huliita solo. Gauni hilo lilificha kila utamu ambao mgeni huyo alifikiri kuyaburudisha macho yake.

"Naitwa Sajini Steven kutoka kituo kidogo cha polisi pale Yombo!" Mgeni akajitambulisha. Mshtuko mdogo ulionekana kwa mwanamke yule. Midomo yake ilimtetema. Steven aliyaona yote hayo kwa Jicho lake la kikazi. "Usiogope!" Akamwambia.
"Ah kuogopa lazima ndugu yangu!" Amina akajibu.
"Nimekuja kwako kikazi..." Akamwonesha kitambulisho, "...lengo hasa ni kutaka kujua kidogo kuhusi kifo cha Bwana Sume..."
"Eh jamani, mwacheni marehemu apumzike..." Amina akajibu huku macho yake yakionekana wazi kuanza kutona machozi.
"Bila shaka! Ila sisi tuliobaki duniani lazima tupambane kuitafuta haki yake..."
"Sawa baba nakusikiliza!" Amina akalainika. Sajini Steven alijua kuongea, kama ni mafuta basi ni yale yenye uwezo wa kulainisha kila kufuri lenye kutu lililogoma kufunguka.
"Ningependa kujua ukaribu wako na marehemu..."
"Ni bwana 'angu!"
"OK... Je unawajua rafiki zake wa karibu?"
"Mmmmm hapana, *any way* kuna baadhi ya wafanyabiashara wenzake ndiyo ninaowafahamu lakini kusema alikuwa na rafiki, yaani rafiki, Sume hakuwa na mtindo huo wa maisha!"

# SHAJARA YA MUUAJI—3



Amina akajibu.

"Na je siku hizi za mwisho uliwahi kumsikia akisema lolote ambalo unaweza kuhisi limesababisha kifo chake?" Sajini Steven alitupa swali ambalo lilimpa Amina jozi la sekunde kutafakari kabla ya kujibu.
"Hapana! Alikuwa kawaida tu..."
"Wala hakuonesha hali ya wasiwasi wowote?"
"Hakuonesha!" Amina akajibu huku akijiweka vema kitini.
"Hebu nambie, ni maeneo gani ambayo marehemu alipenda kutembelea?"
"Sume bwana... Kwanza ujue alikuwa na mke wake wa ndoa..."
"Kwa hiyo we ulikuwa kimada tu?"
"Ndiyo..." Akajibu mkavu.
"Na unamjua mkewe?"
"Ndiyo namjua..."
"Enhe nijibu swali langu sasa!"
"Yule bwana alikuwa akitoka kwenye biashara zake, mawili; ama aende kwa mkewe au aje hapa... Hakuwa na mazoea mengine..."
"Na siku ya kifo chake alitokea wapi?"
"Kwa mkewe... Alikuja hapa saa kumi jioni, tukashinda hapa tukala, tukalalana tena kwa furaha zote... Yaani nimepoteza dume hasa!"
"Kwa sababu alikuwa anajua kazi?"
"Haswa, na hiyo majuzi ilikuwa balaa," Amina alijibu pasi chembe ya aibu.
"Tuyaache hayo!" Steven akamkatisha.
"... Alitoka hapa saa tatu usiku, akaondoka kwenda kwa mke wake. Sume alikuwa na tabia kila asubuhi saa mbili kamili lazima anipigie siku kunijulia hali kama hajalala hapa! Siku hiyo ikawa kimya, nikasubiri na kusubiri wapi! Ikabidi nimpigie. Nilipopiga, simu haipatikani!"
"Ukafanyaje?"
"Kabla sijafanya jingine ndo nikasikia redioni saa nne asubuhi..." Sajini Steven akashusha pumzi na kujiweka sawa. "Sume alikuwa anafanya biashara gani?"
"Alikuwa anasafirisha mazao kutoka mikoani kuleta hapa Dar as salaam..." Amina akajibu.
"Je mliwahi kugombana siku za karibuni?" Sajini Steven akauliza.
Swali hili likawa kama limemshtua kidogo mwanamke yule.

Tsh 4000/= Softcopy. Lipia Mpesa Lipa Namba 5559006 JAMVI LA SIMULIZI. Whatsapp 0766974865

"Ndiyo!" Steven akatulia kidogo akijaribu kuzisoma hisia za Amina, "ilikuwaje? Nisimulie bila kuficha!"
"Yule bwana alikuta meseji ya mapenzi kwenye simu yangu..."
"Ulikuwa na bwana mwingine?"
"Hapana... Sikiliza... Kuna mwanaume mmoja anamiliki *Car Wash* hapo Jet Lumo. Siku moja nilienda pale asubuhi kuosha gari la Sume ambalo huwa natumia. Mi nikashangaa naitwa ofisini, yule bwana *oooh mi sijui nimekuelewa, nakuhitaji eeenh sijui unafaa kuwa na Mimi,* mambo kibao. Nikamwambia nina mtu wangu, aaaah jamaa king'ang'anizi. Basi akasema atanitafuta. Kweli bwana, akachukua namba yangu kwenye rejista yake akaanza kunitongoza kwenye simu. Mara nyingi nilikuwa nafuta zile meseji...

Sasa Siku hiyo sijui hata ilikuwaje! Nikasahau kufuta. Ni yule bwana yani Sume, akihitaji simu yangu anachukua anatumia nami ni nikihitaji kutumia yake natumia... Ilikuwa hivo. Mh! Wakati anatumia akaona ile meseji... Kaka hiki kisebule hakikutosha."

"Pole Amina!" Akampolesha baada ya kuona mwanamke huyo akiongea kwa hisia kali sana mpaka chozi linamtoka.
"Basi bwana! Siku ile amani haikuwepo... Mimi sijawahi kumsaliti yule bwana... Tangu tuanze mapenzi miaka miwili sasa sijawahi kutoka nje. Yule bwana alikasirika... Aliniwasha makofi humu ndani, hakuelewa lolote ninalomwambia. Likapita, mapenzi yakaendelea... Mimi nilimpigia yule bwana wa car wash... Nikamwambia kilichotokea; hasisikitike, akafurahi akasema atahakikisha tunaachana ili anichukue, na alisema atafanya kila awezalo..."

***Itaendelea...***

*Ilipoishia…*

**Aya hiyo ilimaanisha 'Kama tulivyoona katika Mkutano Mkuu, kadiri ya kitabu chetu Chekundu: Ikiwa mmoja wetu anakuwa msaliti ni lazima apotezwe/afutiliwe mbali.**

*Endelea…*

Chini ya maneno hayo kulikuwa na orodha ya majina manne ambayo yaliandikwa kwa wino mwekundu na kuweka msisitizo kuwa, watu hao wanatakiwa kuwa kimya kabisa na wasizungumze lolote linalohusiana na Cronoc 7.


"Sasa kwa nini haya majina yako huku chini ya maneno haya?" Madam akauliza.
"Sijui labda wanatakiwa kuwa eliminated kama ilivyoandikwa hapo juu," Amata akajibu japo hakuwa na uhakika sana.
"Mr. Donald Stephenson wa Australia, Aquald Berret wa Mauritius, Didiof Mathis wa Nigeria na Bi Suzan Oromouf wa Urusi…"
"Wanne hao!" Amata akamkatiza, "majina yao huko juu hayapo, ukiangalia sana hii ni muhtasari wa kikao fulani ambacho mimi na wewe hatujui wapi kimefanyika na haya ni maamuzi ambayo yamepitishwa na jopo hili huku juu ikiwa na maana kwamba hawa wanne hawapo kwenye hiyo program. Ina maana kwamba, ukiacha muhtasari huu kutakuwa na kitu kingine kikubwa na kizito kama si cha hatari na kutisha," Amata akaeleza.
"Nimekupata mwanangu! Sasa hili tuliweke kando, hakikisha unajua kila kitu kuhusu Carlos ikiwezekana upate kilicho kichwani mwake kwa njia yoyote ile, nakupa saa saba tu," Madam S akampa kazi Amata.

"Hiyo imekwisha," akasimama na kuchukua simu yake, akatoka ofisini na kumwacha Madam S peke yake. Moja kwa moja akajitia kwenye gari lake na kuondoka eneo lile.

**07**

SEHEMU fulani, nje ya mji wa Iringa, kengele za kanisani zililia kwa mtindo ambao waumini wa kanisa hilo walijua wazi kuwa hiyo ilikuwa saa kumi na mbili jioni. Katika moja ya barabara ambazo zilikuwa zikielekea katika Monasteri moja iliyojengwa juu ya mlima kulionekana gari lililokuwa likienda kasi sana. Vumbi lililobaki nyuma yake lilitosha kuwaachia wanavijiji waliojenga kando yake vikohozi mfululizo. Ndani ya gari hilo mulikuwa na mtu mmoja, Mzungu, mwenye nywele ndefu akiwa ndani ya vazi la kikasisi. Mwendo ule haukuwa wa kawaida, hakujali kama kuna watoto wala nini. Kila alipopita, watu walishika vichwa.

Kutoka ndani ya mnara wa kengele ya kanisa hilo, kijana mwingine Mzungu aliyekuwa akiigonga na baadae kuifunga kambaye mahali pake, alikaza macho kwenye darubini akiangalia upande wa barabarani ambako gari lile lilikuwa likipita. Kutokana na nguvu ya chombo hicho 'kiona mbali' aliweza kuona sawasawa. Akatikisa kichwa juu chini na kuishusha ile darubini.
"Amewasili," akajisemea kwa sauti ndogo huku akiteremka ngazi kurudi ndani ya nyumba yao ambako aliwaacha wengine.
"Vipi?" mmoja aliuliza.
"Keshafika!"
Ding – Dong! Kengele ya mlango ikalia na kijana mmoja




akaufungua.
"Karibu sana Fr. Bibliot. Pita hapa, umesubiriwa mno," akamkaribisha na kasisi huyo hakujibu, isipokuwa, alifuata maelekezo tu. Akafungua mlango mmoja na kupotelea humo ndani ambako alikutana na mtu mwingine aliyevaa kanzu kama yeye, mzee mwenye nywele nyeupe kichwa kizima na ndevu zake nazo vivyo hivyo. Wawili tu walikuwa ndani humo bila ya mtu mwingine yeyote.

"Karibu mwanangu, karibu sana," yule mzee akamkaribisha mgeni wake. Naye akaketi katika kiti kilichomkabili. Ndani ya chumba hicho hakukuwa na mawasiliano yoyote yaliyokuwa yakitoka nje. Usalama ulizingatiwa kwa kila hali. Hata wawili hao wote simu zao zilizimwa kabisa na eneo hilo lilifungwa mitambo ya kuvuruga mitandao ya simu kiasi kwamba unaweza kumpigia mtu huyu ikapokelewa na mtu mwingine.
"Yes, father… nilikuwa nakusubiri, na najua kuwa unataka kurudi leo hii hii," yule mzee

akamweleza.

"Ndiyo! Sasa nilitaka kukupa taarifa hii kuwa serikali ipo katika uchunguzi mkubwa sana wa swala hili la Bishop Bariki Zebetoni…"

"What?" yule mzee akashangaa, "ina maana hatuaminiani sasa, sivyo?" akaongeza.

"Ndiyo maana nikaomba kuonana nawe. Mpaka sasa wanajua kuwa Askofu yupo London kwa kuwa baada ya uchunguzi wao walikuja pale Kurasini, nasi ndiyo tulikutana nao. Hata hivyo tumejaribu kuwahandle ili kazi yote ibaki upande wetu kwa kuwakumbusha kuwa hata sisi tuna Inteligence Unity katika kanisa," Bibliot akaeleza.

"Ok, sasa fanya hivi, hakikisha unajua nyendo zao zote, na hakikisha una-secure Cronoc 7, iliyo tayari mikononi mwa Zebetoni. Hakikisha isiguswe na mtu awaye yote isipokuwa sisi. Kuhusu hao nitaongea nao waache mara moja uchunguzi wao kwani sisi wenyewe tunaweza kama wanavyodhani, wakiendelea watavuruga mpango wetu," yule mzee akamweleza Bibliot kwa sauti yake kavu na yenye kitetemeshi, "Kuna lingine?" akauliza.

"Ni hayo tu…"

"Sawa ubarikiwe sana katika kazi yako, mimi ninasubiri huo muswada unifikie ili kazi ianze," akambariki.

"Amina!" Bibliot akaitikia na kutoka katika kile chumba, akapita kwenye jokofu na kuchukua kinywaji kikali, akanywa harakaharaka, akachukua simu yake na kuiwasha. Mara tu simu hiyo ilipopata uhai ujumbe mfupi ukaingia.

"…Ulipouacha mzigo sijaukuta…"

Maneno hayo matatu tu, yalimfanya Bibliot kuelewa nini kimetokea, alihisi kama ile pombe inataka kumwagika, akaiwahi na kuweka bilauri vizuri.

"Shiiit!" akaitazama tena ile simu, akajua kuwa hapo hana ujanja wa kuwasiliana na mtu huyo, akaomba moja ya vyumba ambavyo kwavyo mtandao wa simu hupatikana kwa urahisi, akaingia.

"Hello Carlos! Unasemaje?" akauliza kwenye simu.

"Sijaukuta mzigo pale uliponambia, kuna mtu kauchukua kwa kujifanya kuwa yeye ni Carlos," akaeleza.

"Ok, jambo moja tu, deal na huyo mwanamke wa mapokezi, muweke mkononi mwako mpaka nitakapokuja, atatusaidia kuupata, kwaheri," akakata simu na kuitia mfukoni. Kwa njia ya siri akampitishia ujumbe huo yule mzee ambaye yeye alikuwa na maamuzi ya mwisho kabisa katika mambo yao. Bila kuchelewa aliingia kwenye gari lake na kuiacha monasteri ile.

Bibliot alikwenda Iringa kwa jambo la dakika kumi tu, hakuwa anaamini chochote hasa upande wa mawasiliano ya simu kwani alijua wazi kuwa simu zote huwa zinarekodiwa kwa ajili ya usalama. Siku hiyo baada ya kuomba mkutano na Superior wake aliyejichimbia huko Iringa katika eneo tenge la Ilole ndipo alitumiwa ujumbe 'meet me to the Dome at shone'.

Mara tu baada ya kumalizana na mzee huyo akapata taarifa ya kupotea ile bahasha pale Kurasini, taarifa ambayo kwake ilitumwa na Carlos Zejack. Taarifa hiyo ilimchanganya akili alitamani aruke na atue akiwa Kurasini lakini haikuweza kuwa hivyo. Kichwani alijua kuwa ni saa tatu zitakazomgharimu kufika katika jiji la Dar es salaam kwa kuwa ndege ya kukodi ilikuwa ikimsubiri yeye. Saa tatu nyingi sana kiasi kwamba lolote linaweza kutukiai! Alijikuta akiwaza huku akiiacha barabara ya vumbi na kuchukua ile ya lami inayotoka Dar es salaam kwenda Zambia.

*** *** ***

Carlos zejack alishusha kioo cha gari lake aliloliegesha pembeni, jirani kabisa na kituo cha daladala za kwenda Kurasini katika barabara ya Msimbazi.

"Unamuona? Yule paleeee kavaa blauzi nyeupe na skafu ya maua maua…"

"Chini kavaa sketi ya buluu?"

"Yes!" Carlos alikuwa akitoa maelekezo kwa mwanadada aliyekuwa naye ndani ya gari, wakiwa tayari wanamvizia yule mwanadada mfanyakazi wa mapokezi pale hotelini Vatican Wing.

"Nikamlete?" mwanadada aliyekuwa kwenye gari la Carlos akauliza.

***ITAENDELEA...***

**Kitabu cha CRONOC 7—chapa ya pili kitakuwa madukani muda wowote kutoka sasa.**

**Weka oda yako sasa kwa kutuandikia whatsapp 0766974865.**

**Na ukipenda kulipia kabisa waweza fanya hivyo kwa kutuma pesa '12,000/=' kwenda Mpesa Lipa Namba 5559006 JAMVI LA SIMULIZI kisha tutumie meseji ya muamala wako kwa whatsapp hiyo hapo juu.**

# Ya Kale Ni Dhahabu– Alibaba na Wezi 40 (11)

*Inatoka toleo lililopita...*

Akaanza safari ya mjini mpaka sokoni, akaongea na wafanyabiashara mbalimbali hapo sokoni. Akapata taarifa nzuri tu kuhusu mauzo ya kamba, nyama, kuku na vinginevyo pale sokoni, kisha akenda kwenye mgahawa nakuulizia bei ya mkate, kisha akaenda kwenye bustani mbalimbali za pale mjini. Alizungumza na matajiri na pia alizungumza na masikini, alizungumza na mamia ya watu pale mjini lakini hakuweza kupata taarifa yoyote pale mjini. Hakuna mtu yeyote aliyezungumza kuhusu mauaji, wala hakuna yeyote aliyezungumza kuhusu hazina za pangoni.

"Nimezungumza na mamia ya watu lakini hakuna hata mmoja aliyenipa taarifa ya kile ninachokitafuta." Yule mwizi alijisemea mwenyewe. "hakuna hata mtu aliyezunguzia juu ya mtu aliyekufa. Bora tu nirudi kwa kiongozi wangu nimwambie kwamba nimeshindwa. Lakini atakuwa na hasira sana."

Yule mwizi alizunguka mchana kutwa mpaka akachoka. Akaamua kukaa chini karibu na kibanda cha fundi nguo na kuangalia viatu vyake na akaona vimetoboka chini kwa shida ya safari ya mchana kutwa.

Alivivua viatu vile. Kulikuwa na mzee mmoja ndani ya kibanda kile cha fundi nguo, yule mwizi akavipeleka kule ndani.

"Angalia matundu haya kwenye viatu vyangu" mwizi alimwambia yule mzee huku akimuonesha. "Sasa hivi jua litazama, lakini naona kama macho yako hayaoni vizuri mzee, hivi unaona kweli?"

"Ooh!ndio naona matundu haya" alisema Mustafa (fundi nguo). "Macho yangu mazuri tu, mimi ndio fundi nguo maarufu hapa mjini, naona vizuri kiasi cha kuweza kuweka uzi kwenye sindano na kushona. Hakuna mtu hapa mjini anayeweza kushona vizuri kunishinda." Aliendelea kusema. "Na ukizingatia siku chache zilizopita nilikuwa na kazi ngumu sana, nilishona suti ya maiti mmoja katika ghala lenye giza. Ilikuwa ni msichana mmoja wa kazi alikuja na kunipeleka nyumbani kwao kwaajili ya kazi hiyo. Hivyo alinichukua mpaka kwake."

"Maiti!!?" yule mwizi alisema kwa mshangao fulani. Yule mwizi akamsogelea fundi kwa karibu zaidi na kutaka kujizuia na ule mshangao aliouonesha aliposikia kuhusu maiti. "Tafadhali hebu niambie huyo maiti alikufa vipi?" mwizi alimuuliza fundi.

"siwezi kukwambia zaidi kuhusu maiti huyo" fundi alijibu. "Ni siri na nimemuahidi msichana wa watu kuwa nitaitunza siri hii."

Mwizi akachukua sarafu moja ya dhahabu kutoka katika lile vazi lake refu na kumuonesha fundi nguo. "Unaitwa nani mzee wangu?" Mwizi aliuliza. "Mustafa" fundi nguo akajibu.

"Vizuri, Mustafa, sitaki kujua jina la aliyefariki" mwizi alisema huku akitabasamu, "sitaki kujua kitu chochote kuhusu yeye, wewe nipeleke tu nyumbani kwake na nitakulipa vizuri sana."

Mustafa alifikiri kwa muda mfupi kidogo. Kisha akachukua ile sarafu ya dhahabu.

"Nitajaribu" Mustafa alisema, "lakini yule msichana alinichukua hali ya kuwa amenifunga macho na kitambaa hivyo sitaweza kupajua."

"Twende sasa hivi," alisema mwizi. "Utajifunga macho na kitambaa vilevile kama ulivyofanya mwanzo. Vilevile utalazimika kurudi nyumbani katika hali hiyohiyo ili usipajue nyumbani hapo ukaonekana ni mvunjaji wa ahadi. Hata kama utakua huoni wakati tunaenda lakini utatumia harufu za maua na sauti za wanyama kuweza kutambua njia. Jitahidi sana na nitakulipa vizuri sana."

Alipomaliza kusema hayo akachukua sarafu nyingine ya dhahabu na kumuongezea Mustafa. "Nitajaribu," alisema Mustafa huku akitabasamu.

Mustafa akamalizia kushona viatu vya mwizi huyo kisha akafunga kibanda chake. Mwizi akachkua kitambaa kirefu cha njano na kumfunga Mustafa kuzunguka kichwa ili azibe macho yake.

"Sawa kabisa!, sasa jifanye kama ulivyofanya mwanzo" alisema mwizi, "Mimi niwe kama yule msichana wa kazi, sasa jaribu kutafuta sauti njiani na harufu harufu ambazo ulikuwa ukizisikia wakati unapelekwa na yule msichana mara ya kwanza."

***Usikose toleo lijalo...***

# SIMULIZI CLUB YATOA ‘MAOKOTO’

## Yaandaa Tuzo ya Kuinua Waandishi wa Riwaya Nchini

Ni mwezi Mei uliojaa patashika na nguo kuchanika huko kwenye mitandao maarufu ya kijamii; Facebook na Instagram. Hii imetokea baada ya mwanzilishi na msimamizi wa chaneli ya simulizi huko YouTube (Simulizi Club) kuweka wazi nia yake ya kusukuma na kutia moyo na kuinua waandishi chipukizi wa kike na kiume, wazoefu (wale wa kati) wa kike na kiume.

Licha ya hilo pia ametoa nafasi ya kupata Kitabu Bora cha waandishi hao. Na ili hili jambo livute hisia za waandishi na wasomaji, Simulizi Club wameweka kifuta jasho kwa wale wote wataoibuka kidedea katika hilo.

Baada ya kutangaza jambo hilo na kuliweka wazi, waandishi wamepigana vikumbo sana kwa wasomaji wao ili kuomba kura kwa kutumia lugha iliyojaa urai wa kila namna ili kumvuta msomaji huyo kwake. Naweza kusema imewezekana ijapokuwa kweli mchuano umekua mgumu sana.

Jarida pendwa la kifasihi la kila mwezi yaani Ngurumo ya Mwandishi limekuwa likifuatilia tuzo hizo sako kwa bako na vyombo vingine kama Tungo Tata Tv ili kuona hatua kwa hatua ya mchuano huo.

Vipengele vilivyokuwa vikigombaniwa na zawadi zake yaani pesa taslimu ni kama ifuatavyo:-

1. Mtunzi Mzoefu wa Kiume—ambaye mshindi atajinyakulia jumla ya Shilingi za Kitanzania 350,000
2. Mtunzi Chipukizi wa kiume—ambaye mshindi kujinyakulia kitita cha Shilingi za Kitanzani 300,000
3. Mtunzi wa kike—ambaye atajinyakulia Shilingi za Kitanzania 350,000

Ukiachana na vipengele hivyo vya kuwatambua waandishi katika kuishi kwao kwenye tasnia. Pia vilikuwapo vipengele vya kutambua kazi zao kama ifuatavyo:-

1. Kitabu cha Mtunzi chipukizi wa kiume—ambapo mwandishi huyo atajinyakulia kitita cha Shilingi za Kitanzania 230,000
2. Kitabu cha mtunzi wa kike—ambaye mshindi atajinyakulia kitita cha Shilingi za kitanzania 230,000
3. Kitabu cha Mtunzi mzoefu wa kiume—ambapo mshindi atajinyakulia kitita cha Shilingi za Kitanzania 230,000

Licha ya hilo pia, Simulizi Club ilitazama ‘Brand’ ambazo kwa namna moja au nyingine zinaifanya fasihi andishi na simulizi ikue na isambae ndani na nje ya Tanzania na Afrika kwa ujumla. Hiki kilikuwa kipengele pekee ambacho Brand itakayoibuka mshindi basi itajinyakulia kiasi cha Shilingi za Kitanzania 270,000

Pamoja na hayo yote, kwakuwa Simulizi Club huziwasilisha kazi za waandishi kwa hadhira kwa njia ya sauti, palikuwepo na kipengele cha Msimuliaji wa kike na wa kiume ambapo mshindi atajinyakulia Shilingi za Kitanzania 300,000.

“Hili ni jambo la kuigwa sana kwa wale wote wenye uwezo, kuweka Tuzo namna hii si kujionesha kwamba una pesa lakini ni kutoa msukumo kwa waandishi kuona umaana na uzito wa kazi wanazozifanya” alizungumza mshairi na mwanariwaya Shujaa Maneno kutoka Bagamoyo alipohojiwa na jarida hili. Mwanafasihi huyo aliongeza kusema, “Jamii itambue kwamba uandishi ni tasnia inayompa mtu heshima kubwa, kuandika ni kazi ngumu sana, hivyo mmoja anapojitokeza na kuanzisha kitu kama hiki basi wengine wenye uwezo wamdhamini ili kuongeza zawadi kwa wale washindi”.

Kilele cha Tuzo hizi za Simulizi Club kitakuwa tarehe mosi ya mwezi Juni ambapo washindi watatangazwa kupitia mitandao ya Facebook na Instagram na watapatiwa vitita vyao vyenye jumla ya Shilingi za Kitanzania takribani Milioni 2.5

Tuzo hizo zilidhaminiwa na Tulizo Media, Sun Fresh Water LLC na Simulizi Club wenyewe.

Kila la kheri kwa wote waliopenya kwenye kinyang’anyiro hiko.
Ukitaka kuijua zaidi Simulizi Club, tembelea YouTube andika Simulizi Club, au Facebook na Instagram andika Simulizi Club utakutana nao hapo. ***RM***

# SHUBAKA LA VITABU

Katika safu ya SHUBAKA LA VITABU toleo hili la 32, tumembamba Fadhy Mtanga akiwa anapekuapekua kwenye shubaka lake. Na katika upekuzi wake huo anakutana na chambuzi bora sana iliyofanywa na mwandishi mufti kabisa Joseph Shaluwa. Chambuzi hiyo ilikuwa ni juu ya kitabu chake (Fadhy) chenye anwani RAFU. Kwanini Rafu? Hebu tusiklize...

JANA USIKU, KATIKA pitapita zangu mtandaoni, nilikutana na huu uchambuzi wenye miaka minne sasa. Mwandishi maarufu Joseph Shaluwa anayefanya kazi Global Publishers, aliandika kuhusu kitabu hiki. Kimsingi, mimi na Shaluwa tulizindua vitabu vyetu siku moja, mwezi Februari 2020 wakati wa tukio adhimu la fasihi ya Kiswahili, Mjue Mtunzi.

Kwa wakati ule alipochapisha uchambuzi wake, niliusoma. Jana imetokea tu kwa nasibu kwamba, nami nilikuwa nikisoma riwaya yangu ya Rafu nikiwa safarini. Usiku sana ndipo nilipowasili niendako. Miongoni mwa vitu nilivyovifanya wakati nikipigana chenga na usingizi, ilikuwa kuperuzi kumbukumbu za nyuma. Wakati huu nikiwa narudia kusoma kazi yangu ya Rafu, uchambuzi wa ndugu yangu Shaluwa umechochea ashiki ya kitabu hiki.
Nami, pasi kuongeza neno, naomba nikushirikishe alichokiandika.

Aliandika,

SOMA USISIMKE MPAKA BAAAASI!!!
UKISIKIA mwanamke mrembo, uelewe kuwa huyu ninayemzungumzia hapa alikuwa mwanamke mrembo sana. Aliitwa Lina. Ni mfanyakazi. Mwenye mume, ambaye kama yeye alikuwa mfanyakazi.

Aliitwa Kennedy Mwakyoma. Zaidi akijulikana kwa jina la Ken. Walikuwa na mtoto wao mmoja wa kiume. Kai. Ndoa yao ilikuwa ndiyo kwanza ina miaka sita, wakiwa na mtoto anayekaribia umri wa miaka mitatu.
Waliishi maisha mazuri sana yaliyojaa mahaba, mjini Iringa. Lakini siku moja, ghafla tu, kinatokea kitu cha kuwatenganisha wawili hao — KIFO.

Ken anafariki akiwa anatoka kutazama mechi ya timu yake aipendayo, Arsenal. Taarifa za kifo hiki zinapokelewa na Lina na wifi yake, Edna, ambao walifika kituo kikuu cha polisi, Iringa kutoa taarifa ya kupotelewa na ndugu yao. Maelezo wanayoyapata baadaye ni kuwa Ken alifariki ghafla baada ya kupata kiharusi.
Familia nzima ilikubaliana na ripoti hiyo ya daktari, kuwa Ken alikufa kwa kiharusi.

Lakini Lina anakataa. Anahisi kuna kitu. Hatimaye Ken alizikwa, lakini Lina akaamua kutumia misemo ya marehemu mume wake “Siku zote ziamini hisia zako” na “Uliza kila kitu”, kuanza kufanya uchunguzi wa kimyakimya kwa kutumia mbinu zake mwenyewe! Ni mbinu hatari, lakini hakuogopa. Alitaka kutetea haki ya uhai wa mumewe kuondolewa!

Ufukunyuzi wake unazalisha hadithi nyingine nzuri sana isiyochosha kusoma. Kunakuwa na pilika nyingi, za usiku na mchana. Vicheko na huzuni. Uoga na kujiamini.

Mchakamchaka wa nguvu ambao unamfichulia ukweli wa kifo cha mume wake mpendwa Ken. Anagundua kuna RAFU ilichezwa ili kumpoteza mumewe.

Pilikapilika hizi anazifanya kwa kushirikiana kwa karibu na wifi yake Edna, ambao walipendana, kuzoeana, kuheshimiana, kuaminiana kusiko na kipimo, kiasi cha kuamua kuanza kuitana dada.
Sasa vuta picha, mtu na wifiye ambao imezoeleka huwa maadui, hawa wanaitana dada! Ni ushosti wa nguvu kiasi gani?

Stori hii tamu utaisoma kama sinema ya kusisimua, ikikufundisha mitaa na sehemu mbalimbali za mjini Iringa, Mbeya, Morogoro, Arusha, Malawi na Dar es Salaam.

Lakini stori inakwenda kuishia jijini Kampala, Uganda. Unajua ni kitabu chenye jina gani? RAFU. Mwandishi ni FADHY MTANGA.
Fuatana nami kwenye uchambuzi wa sehemu muhimu japo kwa
uchache:

*Usiikose Toleo lijalo...*



# KITABU NILICHOSOMA

## Who Will Cry When You Die




Maktaba: Anna Mbise Mobile Library
**Kitabu:** WHO WILL CRY WHEN YOU DIE (NANI ATALIA SIKU UKIFA)
**MWANDISHI:** ROBIN SHARMA
**MSOMAJI:** ERICK MBISE:
**MKOA WA MSOMAJI:** ARUSHA.

***Kutoka toleo lililopita...***
**5. _Tumia siku yako bila kuwa na saa;_**
" **I _need to be human being rather than being human doing** " Kuna wakati tunatakiwa kuwa binadamu na kuishi maisha ya furaha siyo kila saa tunatazama wakati na kukimbizana na muda. Mwandishi anasema aliondoka nyumbani bila saa na kufanya anachotaka bila kutazama muda ila kufanya anachotamani kufanya. Anasema ilikua siku ya furaha, ni kweli wengi tunatazama sana muda na tumekua watumwa wa maisha yetu wenyewe.

**6. *Kuishi maisha ya Kusamehe,***
Kumsamehe mtu aliyekukosea ni kitendo cha mtu binafsi kuliko kujitolea. Kuachana na uadui na chuki ambayo unaweza kuwa umeiruhusu kuingia ndani yako ni kitu ambacho unajifanyia mwenyewe badala ya faida ya mtu mwingine. Chuki dhidi ya mtu, ni kama unambeba mtu huyo mgongoni mwako anakumaliza nishati yako, shauku na amani ya akili. Lakini mara tu unapomsamehe, unamtoa nyuma yako na unaweza kuendelea na dunia nzima.

Mark Twain aliandika kwamba, " **Msamaha ni harufu nzuri ambayo urujuani humwaga kwenye uponyaji uliouponda."**

Msamaha ni tendo kubwa la roho na ujasiri wa kibinafsi. Pia ni mojawapo ya njia bora za kuinua ubora wa maisha yako. nimegundua kuwa kila dakika unayojishughulisha kumfikiria mtu aliyekukosea ni dakika umeiba kutoka kwa harakati inayofaa zaidi kuvutia watu hao ambao watakusaidia.

7. ***Siyo kila kitabu unachochukua kusoma unatakiwa kumaliza kukisoma;***
Fracis Bacon alivyosema, "Vitabu vingine vinapaswa kuonja, vingine kumezwa, na vingine vichache kutafunwa na kusagwa: yaani, baadhi ya vitabu vinapaswa kusomwa kwa sehemu tu, vingine visomwe, lakini si kwa udadisi, na baadhi ya vitabu vichache vya kusomwa kabisa, na kwa bidii na mvuto.". Hii ina maana katika maisha ya kawaida hata nje ya vitabu ukiondoa dhana ya kitabu hii point inakua na nguvu. Siyo kila jambo utaenda nalo hadi mwisho, siyo kila mtu utaenda naye hadi mwisho. Hii inaweza pia kuwa dhana ya mipaka.

8. ***Usiwe na wasiwasi juu ya mambo ambayo huwezi kuyabadili.***
Kuna mambo yalivyo ni ngumu kuyabadili ila tunatakiwa kukubali na kuendelea. Siyo kila jambo tutakubali haliwezekani ila kuna mambo inafika wakati unakubali kwamba hayawezi tena kubadilika. Waswahili husema maji yakishamwagika hayazoleki.

**9. *Kuishi kwa ajili ya wengine;***
Mara nyingi tunapambana kwaajili ya maisha yetu tu lakini ili maisha yakamilike lazima tuwajali wengine.

Albert Schweitzer alisema, "Hakuna dini ya juu kuliko huduma ya kibinadamu. Kufanya kazi kwa manufaa ya wote ni imani kuu . Nilivyosoma hapa nikakumbuka maneno matakatifu ya Biblia "Mpende jirani yako kama nafsi yako"

Jifunze kuwahudumia watu na kuongeza thamani kwa ulimwengu siku ukiondoka hao watu watalia kwaajili yako.

Akitolea mfano Mahatma Gandhi Katika hadithi moja ya kukumbukwa kutoka kwa maisha yake, yeye alikuwa akisafiri kuvuka India kwa treni. alipoliacha gari alilopanda, kiatu chake kimoja kilianguka Sehemu ambayo hawezi kukichukua badala ya kuhangaika kukitafuta alifanya jambo ambalo liliwashtua wenzake wasafirio: alivua kiatu chake kingine na kukitupa pale kilipotulia cha kwanza. alipoulizwa kwanini alifanya hivyo, Gandhi alitabasamu na kujibu: "Sasa mtu maskini ambaye atapata wa kwanza atakuwa na jozi anayoweza kuvaa."

**_10. *Kuwa Mzazi bora;***
Katika hiki kitabu nimejifunza nitakavyolelea watoto wangu vizuri ndivyo ninatengeneza kizazi bora hata baada ya kuondoka Duniani ila nitaacha kizazi bora ambacho kilipata misingi mizuri. Though sijaoa ila nimeanza kupata somo baadae Mungu akipenda nikija kuwa baba nimkumbuke Robin Sharma. Nipate muda wa kukaa na watoto na kuwalea katika njia ipasayo. Watoto ni zaidi ya kazi na mihangaiko yote ya maisha.
***Asante!***



FROMA Liquid Detergent







- **Tunauza Multipurpose Soap jumla na rejareja.**
  **Lita 3 kwa Tsh 3,000**
  **Lita 5 kwa Tsh 10,000**

- **Tunauza mitandio ya kisasa kwa akinadada na akinamama wa kileo Tsh 10,000**

- **Tunauza mataulo mazuri sana, kwa rika zote Tsh 15,000**





**Tunapatikana**
**Dar es salaam**
**KIMARA BARUTI.**
**Mikoani tunatuma.**

**Mawasiliano:**
**Simu: 0654899743**
**Instagram: froma1326**

**Karibu tukuhudumie!**

TANGAZA na NGURUMO YA MWANDISHI kwa bei nafuu na ya kirafiki.
Matangazo madogo ni Tsh 5000@ na Tangazo la kurasa nzima ni Tsh 10000@.
Wasiliana nasi kwa simu *(call & Whatsapp)* 0766974865 na Email: jamvilasimulizi@gmail.com

## TUTAFIKA?

Hali yawa mbaya
Kuliko kazi ya yaya
Watu waishi pasi haya
Kuwafanyia wenzao ubaya

Rushwa hospitalini
Rushwa maofisini
Vipi wale masikini
Msaada awape nani

Nenda hospitalini,
Hakuna hata kwinini
Panado aspirini
Kaweka kwake garini

Nenda upolisini
Yaleyale yumkini
Nduguyo awekwa ndani
Hatoki pasi kitu mkononi

Na huko uajirini,
Kumeoza masikini,
Kama huna kimini,
Dada huingii kazini,

Huko barabarani,
Trafiki polisi jamani,
Kosa lahusu faini,
Taambiwa lipa tu ya njiani,

Hata huko TAKUKURUni,
Nani wa kumwamini,
Jamani mwatusaidiani,
Sisi tulo huku chini?

Tutafika?

**Na: Shujaa Maneno**
**Bagamoyo Pwani**

## KUMBUKA ULIPOTOKA.

Moyo waninyong'onyea, furaha imetoweka.
Vijana wanapotea, mijini wanapofika.
Ugenini walowea, kwao pasahaulika.
Kijana unakosea, kumbuka ulipotoka

Pesa ukishazishika, nyumbani unasahau.
Pindi ukihitajika, wito unaudharau.
Kwani utafilisika?, kurejea angalau.
Kijana unakosea, kumbuka ulipotoka.

Sitowacha kuongea, hata kama waudhika.
Meza pombe meenea, wanywa hadi watapika.
Wazazi walokulea, nyumbani wataabika
Kijana unakosea, kumbuka ulipotoka

Pesa nyingi watapanya, vilabu unapokwenda.
Mama anakosa nyanya, kutia kwenye mlenda.
Jamii waidanganya, wazazi unawapenda.
Kijana unakosea, kumbuka ulipotoka.

Nyumbani baba ahenya, kuzifyatua tofali.
Mamio kuni agwenya, maji afuata mbali.
Miguuni inapenya, miba yenye ncha kali.
Kijana unakosea, kumbuka ulipotoka


Mambo gani unafanya, ndugu yangu nakuasa.
Usikie nakukanya, siendekeze anasa.
Pesa hizo wakusanya, kuzitunza yakupasa.
Kijana unakosea, kumbuka ulipotoka

Hima utafute mwanya, kawone baba na mama.
Kuwa na fikara chanya, imara utasimama.
Sitarehe kuchanganya, mambo yako yatakwama.
Kijana unakosea, kumbuka ulipotoka.

**Na. Jane Davis Mwaninzua**
**E-mail: jmwanizuwa@gmail.com**

**Unaweza kuchangia chochote ili kuwezesha jarida hili kuwa bora na kuwafikia wengi zaidi. Kama upo tayari, changia kiasi chochote kupitia MPESA LIPA NAMBA 5559006 JAMVI LA SIMULIZI. Na Mungu atakujazi.**

# Habari Picha



Mwandishi Mwamwingila na Hussein Wamaiywa katika picha ya pamoja na Mh. Ndumbaro (MB) Waziri wa Sanaa, Utamaduni na Maichezo



Katika picha ya pamoja, Mwandishi Mwamwingila GP na Waziri wa Sanaa, Utamaduni na Michezo Mh. Damas Ndumbaro (MB)




**Bi. Doreen Sinare, Mtendaji Mkuu wa COSOTA akiwa na Mwandishi Mwamwingila GP (Mtalimbo Books) wakati wa uzinduzi wa kampeni ya kuelekea uzinduzi wa Bima ya Penzi katika Hoteli ya Jphari Rotana Dar es salaam.**

# KUTOKA MAKTABA: MAISHA NI MAPAMBANO—1

**Hiki ni kitabu kilichoandikwa miaka mingi sana nyuma. Kiliandikwa ili kiweze kusomwa na watu mbalimbali na kuwekwa kwenye maktaba za vijijini. Tunakitoa kutoka kwenye maktaba yetu ili kukupa uhondo, Ngurumo ya Mwandishi ni kisima cha fasihi chenye hazina iliyotukuka.**

**MSIMULIZI wa hadithi hii ni ndugu Mpepo wa kijiji cha Tetere mkoani Rukwa. Yeye ana umri wa miaka thelathini na tano (wakati huo) na ameoa. Habari za maisha yake kwa ujumla zinajitokeza ndani ya hadithi yenyewe. Ili masimulizi yake yasiathirike, hebu tumsikilize yeye mwenyewe anatuambia nini katika sura hii ya kwanza.**

## SURA YA KWANZA
### Uamuzi wa watu wazima

"Baada ya mkusanyiko ule kuvunjika kila mmoja alielekea nyumbani kwake. Makundi yalikuwa ya watu wawili, wawili, na pengine kufuatana na kila mmoja alivyopenda. Wengine waliamua kutofuatana na yeyote. Mimi nilikuwa mmoja ambaye siku wa na mvuto wa kufuatana na mtu mwingine. Wote tulikuwa na tunatoka kiatika mashauri yaliyohusu ugonvi uliotokea kati yangu na Selemani.

Ilipodhihirika kuwa nilikuwa na makosa ya kupigana ingawa nilichokozwa, iliamuliwa nitulize hasira za wazee kwa mtungi wa pombe. Naye Seremani nimlipe kondoo mnono ili amle na kurudisha damu nyingi aliyopoteza katika pambano lile haramu. Hapa kwetu Tetere ni jambo linalokubalika kuwa wazee wanaloamua halipingwi. Mimi nilikubaliana na uamuzi huo ingawa moyoni nilikuwa na shaka kidogo. Hata hivyo hapakuwa na kinyume. Kama mambo yangelipelekwa mahakamani, ningejuta. Potelea mbali, yabaki yalivyo. Mkasa wote uliotokea baada ya kutaka kumwadhibu mtoto wa Selemani kwa kosa la kuchunga mifugo yao shambani mwangu.

Ugovi ulianza wakati ule Selemani aliponikuta nimemshika mwanawe. Bila kuuliza, yeye alinirukia na kuniwahi midundo miwili juu ya paji langu la uso kwa kutumia kichwa. Maumivu yaliyonipata sikudhani kichwa cha mtu kingeweza kutumiwa kwa kazi mbaya namna hiyo. Mwanaume sikuridhika nikamkamata na kumbwaga mweleka. Mtu kupigwa bila kosa ni kitendo kinachoweza kuleta maafa makubwa.

Baada ya kumbwaga pale chini, bila kufahamu nitendalo nilianza kumtoa nyama kwa kutumia meno na nguvu nyingi. Kazi ya kurarua mwili wa mtu si rahisi, lakini mimi nilifanikiwa. Bidii ya mikono ya selemani na mateke yake mengi hayakunizuia. Wazo likanijia nimtoa macho ndiyo niondoke. Bahati haikuwa yangu, nilishtuka nilipokamatwa na mtu nguvu na kuachanishwa na mgonvi wangu. Kumbe yule mtoto wake alikuwa amekwenda kuwaita watu waje kusaidia kuamua ugonvi ule

Siku ile ilikuwa ya balaa kwelikweli. Kwa kuogopa mambo yaliyotokea yasirudiwe tuliwekwa mbalimbali. Iliamuliwa tupatanishwe. Ndivyo mambo yalivyokuwa.

Katika maisha yangu ya siku za nyuma sikuwahi kupigana, hata katika utoto wangu. Hili pambano langu la kwanza limenipa mauto mengi. Selemani naye, ingawa mara kwa mara hakosi kupigana, hii ilikuwa mara yake ya kwanza kuondolewa sehemu ya nyama kutoka kwenye shavu.

Tangu nisaliwe sasa yapata miaka thelathini na tano. Mke wangu mpenzi nilimwoa miaka mitatu iliyopita. Hivi sasa yeye ni mama Tabu kwa binti yetu tuliyempata miezi michache iliyopita.

Niliporejea nyumbani alikuwa na huzuni akijaribu kutabiri yaliyonipata kule nilikotoka. Hii inadhihirisha kwamba mwenzako apatwapo na mkasa wewe huguswa vilevile. Kinyume cha hivyo basi huyo si mwenzio. Huzuni niliiiona na kuisoma katika uso wake. Nisielewe la kufanya, tukabaki kutazamana.

Mama Tabu alipoona nimekuwa mtulivu mno alianza kulia, huku akipiga kwikwi za mara kwa mara. Loo tabu gani ile? Nikaona nimefanya vibaya kwa kuchelewa kumweleza. Kuanza kumweleza ikawa vigumu nikihisi kwamba nitamwumiza moyoni. Midomo haikufahamu ingejizungushaje ili kutoa matamshi. Baada ya muda kidogo nilijikuta naloa kifua changu…

***Itaendelea toleo lijalo...***

# Ukamataji, Upekuzi na Dhamana ya Polisi—3

## Upekuzi

***Ibara ya 12:- Usawa wa Binadamu***

12(1) Binadamu wote huzaliwa huru na wote ni sawa

12(2) kila mtu anastahili heshima ya kutambuliwa na kuthaminiwa utu wake.

Ibara ya 16: Haki ya faragha na usalama wa mtu

16(1) Kila mtu anastahili kuheshimiwa na kupata hifadhi ya nafsi yake binafsi na familia yake na unyumba wake, na pia heshima na hifadhi ya maskani yake na mawasiliano yake binafsi.

16(2) Kwa madhumuni ya kuhifadhi haki ya mtu kwa mujibu wa ibara hii, mamlaka ya nchi itaweka utaratibu wa sheria kuhusu hali, namna na kiasi ambacho haki ya mtu ya faragha na ya usalama na nafsi yake, mali yake na maskani yake yaweze kuingiliwa bila kuathiri ibara hii.

Ibara ya 24: Haki ya kumiliki mali

24(1) Bila kuathiri masharti ya sheria za nchi zinazohusika, kila mtu anayo haki ya kumiliki mali, na haki ya hifadhi kwa mali yake kwa mali yake kwa mujibu wa sheria.

24(2) Bila kuathiri masharti ya ibara ndogo ya (1), ni marufuku kwa mtu yeyote kunyang'anywa mali yake kwa madhumuni ya kuitaifisha au kwa madhumuni mengineyo bila idhini ya sheria ambayo inaweka masharti ya kutoa fidia inayostahili.

AINA ZA UPEKUZI

Upekuzi unaweza kuugawanya katika sehemu kuu mbili ambazo ni:-

i. Upekuzi unaofanyika baada ya hati ya upekuzi kutolewa.

ii. Upekuzi unaofanyika bila hati ya upekuzi.

UPEKUZI MAUNGONI

Kifungu cha 24 cha sheria ya mwenendo wa makosa ya jinai, kinampa mamlaka na uwezo afisa wa Polisi kufanya upekuzi maungoni mwa mtu yeyote aliyemkamata.

Upekuzi huo unafanyika mara tu baada ya mtu kukamatwa na kuwa chini ya ulinzi.

Kifungu hiki pia, kinampa uwezo wa kuchukua toka maungoni mwa mtu huyo kitu chochote cha hatari au kitakachosaidia upelelezi wa tuhuma zilizosababisha kukamatwa.

Kwa kawaida upekuzi wa maungoni hurudiwa tena, pale mtuhumiwa anapofikisha kituo cha polisi.

Upekuzi wa awamu hii, mtuhumiwa hupewa hati ya kuthibitisha vitu vilivyokutwa maungoni mwake, ambavyo kisheria kama atalazimika kuwekwa katika mahabusu ya Polisi hatoruhusiwa kuwa navyo.

Vitu ambavyo mtuhumiwa haruhusiwi kuingia navyo mahabusu ni pamoja na:- Pesa, simu, mkanda, kamba, silaha, viatu nk.

**UPEKUZI WA MWANAMKE**

sheria inatoa umuhimu wa kipekee kwa mwanamke pale tendo la upekuzi linapotakiwa kufanyika dhidi yake. Aidha iwe maungoni au hata kwenye makazi yake.

Kifungu cha 26 cha sheria ya mwenendo wa ma-

kosa ya jinai, kinatoa ufafanuzi wa jinsi mwanamke atakavyopekuliwa. Kwamba upekuzi huo sharti ufanywe na Polisi mwanamke.

Lengo la sharti hili ni kulinda ***utu na hadhi*** ya mwanamke. Lakini kama hakuna afisa wa Polisi mwanamke, afisa anayehusika na zoezi hilo anaweza kumwelekeza mwanamke yeyote mwenye akili timamu aliye karibu akafanya upekuzi huo kwa niaba.

Vilevile katika mazingira ya ukamataji, kama afisa wa polisi ataamini au kuhisi maungoni mwa mtuhumiwa aliyekamtwa (ambaye ni mwanamke), kunaweza kukawepo kitu cha hatari kama vile:- Silaha au kitu chochote kinachohusiana na upelelezi au silaha inayoweza kutumiwa na mwanamke huyo kufanya shambulio au kitu kinachoweza kupotezwa au kuharibiwa ili kuathiri upelelezi au ushahidi.

sheria inampa uwezo afisa wa Polisi mwanaume kunyakua kutoka katika maungo ya mwanamke huyo kitu au vitu hivyo.

YAFUATAYO NI MAMBO MUHIMU YANAYOZINGATIWA KATIKA UPEKUZI

1) Kutokana na unyeti wa tendo la upekuzi, ni vyema kabla na baada ya upekuzi kufanyika afisa wa Polisi au mtu mwingine anayefanya upekuzi akawa na mashahidi wa kushuhudia upekuzi huo. Si lazima shahidi awe mjumbe au mwenyekiti ama katibu au diwani au kiongozi yoyote wa serikali. sheria inaeleza kwamba mtu yeyote mwenye akili timamu anaweza kuwa shahidi wa tendo hilo la upekuzi.

2) Ni haki ya msingi kabisa ya mmiliki wa nyumba, jengo au eneo linalotakiwa kupekuliwa ***kuoneshwa*** na ***kuona HATI*** inayoidhinisha upekuzi, ***pia ni muhimu mashahidi waione hati*** hiyo kabla upekuzi huo haujafanyika.

3) Mara baada ya tendo la upekuzi kufanyika, afisa wa Polisi atawataka mashahidi walioshuhudia upekuzi na mmiliki wa eneo lililofanyiwa upekuzi ***watie sahihi kwenye hati ya upekuzi,*** ili kuthibitisha kwamba upekuzi umefanyika kwa kufuata taratibu na kwamba vitu au kitu kilichokuwa kitafutwa kimepatikana au hakijapatikana.

4) Kama upekuzi umefanyika bila hati, au hati iliyoidhinisha upekuzi huo haina nafasi ya mashahidi na mmiliki kutia sahihi zao, afisa wa Polisi ataandika hati maalumu ya kuthibitisha upekuzi huo ikionesha kupatikana au kutopatikana kwa kitu au vitu vilivyokuwa vinatafutwa kwenye eneo hilo na mmiliki na mashahidi watatia sahihi zao kwenye hati hiyo na wao kupewa nakala ya hati hiyo.

5) sheria inampa uwezo afisa wa Polisi wakati wa upekuzi, kuchukua kitu au vitu vyovyote atakavyovitilia shaka kwenye eneo hilo, hata kama havikuorodheshwa kwenye orodha ya vitu au kitu kinachotafutwa. Lakini shaka hiyo lazima iwe ya msingi kwa sababu si halali kwa afisa wa Polisi au mtu yeyote anayefanya upekuzi kutaifisha mali ya mmiliki wa kisingizio chochote kile na kufanya hivyo ni kosa.

6) Kitu au vitu vitakavyopatikana wakati wa upekuzi ni sharti vikabidhiwe katika kituo cha Polisi au Mahakamani. Kama huduma zote mbili hazipo karibu, afisa wa Polisi au mtu yeyote aliyefanya upekuzi atavikabidhi vitu hivyo kwenye ofisi ya serikali ya kijiji ili viwe chini ya ulinzi. Si halali kwa afisa wa Polisi au mtu yeyote, kuhifadhi vitu au kitu kilichopatikana kwenye upekuzi nyumbani kwake au mahali pengine popote pasipo salama ili kuepuka ushahidi kuharibiwa.

***Itaendelea toleo lijalo….***

**Tangazo**




www.richardmwambe.com
JAMVI la SIMULIZI

Jarida hili hutolewa na Jamvi la Simulizi kila mwezi
jamvilasimulizi@gmail.com